

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**TANZIA**



**MAREHEMU FRANCISCA MATHAYO HAULE**

**17/09/1987 – 11/07/2022**

Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndg. Nanelwa Mwihambi *ndc*, anasikitika kutangaza kifo cha Mtumishi wa Ofisi ya Bunge Ndg. Francisca Mathayo Haule, Afisa Utafiti Mwandamizi kilichotokea tarehe 11 Julai, 2022 katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, Jijini Dodoma alikokuwa akipatiwa matibabu.

“Nimepokea kwa masikitiko taarifa ya msiba huu wa Mtumishi mwenzetu. Natoa pole kwa familia, Watumishi wa Bunge, ndugu, jamaa na marafiki. Mwenyezi Mungu ampe pumziko la milele na kutufaraji sote”.

Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na familia ya Marehemu inaratibu mipango ya mazishi yanayotarajiwa kufanyika Ijumaa tarehe 15 Julai, 2022 Mtwara Mikindani.

Mungu ailaze Roho ya Marehemu Mahala pema peponi, Amina.

Imetolewa na: Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,  
Ofisi ya Bunge,  
**DODOMA.**

12 Julai, 2022

